| | |
|---|---|
| Title | Miundo ya Sentensi za Njeo Iliyopita katika Kitumbatu-Gomani : Kwa Kulinganisha na Kichaani na Kiswahili Sanifu |
| Author(s) | Takemura, Keiko |
| Citation | スワヒリ＆アフリカ研究. 2017, 28, p. 109-121 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/66408 |
| rights | |
| Note | |

*Osaka University Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

Osaka University

『スワヒリ＆アフリカ研究』28 号（2017）109-121
大阪大学大学院言語文化研究科スワヒリ語研究室発行

# Miundo ya Sentensi za Njeo Iliyopita katika Kitumbatu-Gomani

## - Kwa Kulinganisha na Kichaani na Kiswahili Sanifu -

TAKEMURA Keiko

## 0. Utangulizi

Kama tulivyohakikisha katika makala ya Takemura (2014, 2015 na 2016), ingawa Kiswahili kina lahaja nyingi kiasi na hata baadhi ya lahaja hizo tayari zimeshafanyiwa tafiti nyingi (Stigand 1915, Bryan 1959, Mkude 1983, Nurse & Hinnebusch 1993, Stude 1995), mengi yanayohusiana na sarufi za lahaja hizo bado hayajafafanuliwa vizuri.

Na kama nilivyoandika katika makala nyingine (Takemura 2014, 2015 na 2016), mimi mwenyewe nimefanya utafiti wa lahaja kadhaa za Kiswahili[1)] kwa muda wa miaka 20 hivi katika Mkoa wa Kaskazini, kisiwani Unguja. Lahaja niliyofanyia utafiti zaidi ni Kichaani yaani Kiswahili kinachozungumzwa katika kijiji kinachoitwa Chaani. Na kijiji hiki kimetambulikana kuwa kilijengwa na watu wanaotoka kisiwa cha Tumbatu, basi Kiswahili kinachozungumzwa kijijini hapo ni tawi moja la lahaja hasa ya Kitumbatu. Kwa kweli wengi wa wanaoishi katika kijiji hicho wametanabahi kwamba Kiswahili wanachosema kinatofautiana na Kiswahili Sanifu na kinafanana na Kitumbatu. Kutokana na matokeo ya utafiti wangu vilevile imethibitishwa kuwa Kichaani na Kiswahili Sanifu kinatofautiana hata kisarufi na kimsamiati, na lahaja za Kichaani na Kitumbatu zinafanana (Takemura 2014, 2015 na 2016).

Lakini mpaka sasa bado sijalinganisha vizuri Kichaani na Kitumbatu na tena kwa bahati mbaya sijakamilisha utafiti wangu hasa juu ya Kitumbatu. Mwaka uliopita 2016 nilibahatika kuanza utafiti juu ya Kitumbatu-Gomani kwa kupata msaada wa mhojiwa ‘M’ aliyezaliwa Gomani, kisiwa cha Tumbatu. Bado niko njiani tu katika kufafanua sarufi ya lahaja hiyo, lakini katika makala hii tutaangalia miundo ya sentensi za njeo iliyopita ili kubainisha tofauti kubwa baina ya Kitumbatu-Gomani na Kiswahili Sanifu na ulinganifu baina ya Kitumbatu-Gomani na Kichaani. Kwanza tutazungumzia muundo wa dhamira dhahiri katika Kitumbatu-Gomani. Na tunapoandika Kitumbatu-Gomani, tunafuata kanuni ya kuandika Kiswahili Sanifu. Ili kubainisha tofauti baina ya Kitumbatu-Gomani na Kiswahili Sanifu na Kichaani, tutaonyesha mifano ya sentensi za Kitumbatu-Gomani na Kichaani pamoja na tafsiri zake kwa Kiswahili Sanifu. Mifano yenye herufi

[1)] Nimefanya utafiti wangu huko kijijini Chaani tangu mwaka 1997 mpaka mwaka 2016. Hata mwaka huu 2017 pia natarajia kuendelea na utafiti wangu. Na utafiti huu mzima unasaidiwa na bajeti maalum ya kirasmi inayotokana na JSPS.

‘a’ ni sentensi za Kitumbatu-Gomani, na yenye herufi ‘b’ ni sentensi za Kichaani[2)], na yenye herufi ‘c’ ni sentensi za Kiswahili Sanifu. Na tafsiri za sentensi hizo kwa Kiingereza zinaambatanishwa juu.

## 1. Muundo wa Dhamira Dhahiri

Katika Kitumbatu-Gomani, muundo wa dhamira dhahiri ni hivi:

| kiambishi-kiima – kiambishi-njeo – kiambishi-yambwa – mzizi wa kitenzi – kiambishi-nyambulishi – kiishio |
|---|

(1) ‘You write a letter to me.’

a. Ku-na-ni-andik-i-ya baruwa.
SM2SG-PRS-OM1SG-write-APPL-BF letter9

b. Ku-na-ni-andik-i-ya baruwa.
SM2SG-PRS-OM1SG-write-APPL-BF letter9

c. U-na-ni-andik-i-a barua.
SM2SG-PRS-OM1SG-write-APPL-BF letter9

Katika muundo huu, kiambishi-kiima, kiambishi-njeo, mzizi wa kitenzi na kiishio ndizo mofimu za msingi zisizokosekana. Kiambishi-kiima kinatokea kupatana na kiima cha sentensi na kiambishi-yambwa kinatokea kupatana na yambwa ya sentensi, lakini baadhi ya sentensi hazina kiima chenyewe wala yambwa yenyewe. Basi katika sentensi kama hizo kiambishi-kiima na kiambishi-yambwa kinafanya kazi ya kiwakilishi hasa ikiwa kiambishi-kiima ama kiambishi-yambwa ni kiambishi-nafsi. Katika sentensi kiwakilishi-nafsi hakitokei kwa kawaida, na kikitokea kinafanya kazi ya kusisitiza.

Ikiwa nomino ya kiima ama ya yambwa ina maana ya ‘kiumbe’, hata kama nomino hii si ya ngeli ya 1 (umoja) au ya 2 (wingi), kiambishi-kiima ama kiambishi-yambwa sharti kiwe cha ngeli ya 1 au ya 2. Ikiwa sentensi yenyewe ni ya kukanusha, kiambishi-kiima lazima kiwe cha kukanusha.

## 2. Muundo wa Sentensi za Njeo Iliyopita

Sasa tuangalie sentensi za njeo iliyopita. Tutatazama muundo wake katika ngeli mbalimbali ili kuhakikisha kama kuna tofauti baina ya sentensi zenye kiima ‘kiumbe’ na kiima ambacho ‘si kiumbe’.

[2)] Muundo wa sentensi za Kichaani umeonyeshwa katika makala yangu ya 2015 na 2016.

## 2.1 Kitenzi chenye Silabi Zaidi ya Mbili

(2) 'I laughed'

a. ni-chek-e
SM1SG-laugh-V

b. ni-chek-e
SM1SG-laugh-V

c. ni-li-chek-a
SM1SG-Pst-laugh-BF

(3) 'you laughed'

a. ku-chek-e
SM2SG-laugh-V

b. ku-chek-e
SM2SG-laugh-V

c. u-li-chek-a
SM2SG-Pst-laugh-BF

(4) 'we saw her/him'

a. tu-m-on-o
SM1PL-OM3SG-see-V

b. tu-m-on-o
SM1PL-OM3SG-see-V

c. tu-li-mw-on-a
SM1PL-Pst-OM3SG-see-BF

(5) 'a child bought a book'

a. mwana ka-nunu-ɭu kitabu
child1 SM3SG-buy-V book7

b. mwana ka-nunu-yu buku
child1 SM3SG-buy-V book5

c. mtoto a-li-nunu-a kitabu
child1 SM3SG-Pst-buy-BF book7

Kama tunavyoona katika sentensi zilizoonyeshwa juu, muundo wa kitenzi katika sentensi za Kitumbatu-Gomani na Kichaani katika njeo iliyopita lazima uwe na kiambishi-tamati chenye vokali sawa na vokali iliyopo mwishoni mwa mzizi wa kitenzi. Na kiambishi-njeo hakipo katika Kitumbatu-Gomani na Kichaani ingawa Kiswahili Sanifu kina kiambishi-njeo cha wakati uliopita '-li'. Na isitoshe, kiambishi-tamati cha Kitumbatu-Gomani na Kichaani kinayo konsonanti moja[3)] kabla ya vokali ili kuepusha mfululizo wa vokali tatu wakati mzizi wa kitenzi unapoishia na vokali.

Sasa tuangalie kauli ya ukanushi ikoje.

---

[3)] Ingawa bado hatujafanya utafiti vizuri juu ya konsonanti zote za Kitumbatu-Gomani, lakini tuseme kwa hapa katika Kitumbatu-Gomani inatumika konsonanti [ɭ], na katika Kichaani inatumika konsonanti [j]. Katika makala hii tunaonyesha konsonanti [ɭ] kwa herufi ɭ.

(6) 'I didn't laugh'

a. si-e-chek-a (> secheka)
NegSM1SG-NegPst-laugh-BF

b. si-e-chek-a (> secheka)
NegSM1SG-NegPst-laugh-BF

c. si-ku-chek-a
NegSM1SG-NegPst-laugh-BF

(7) 'you didn't laugh'

a. hu-e-chek-a (> hwecheka)
NegSM2SG-NegPst-laugh-BF

b. hu-e-chek-a (> hwecheka)
NegSM2SG-NegPst-laugh-BF

c. hu-ku-chek-a
NegSM2SG-NegPst-laugh-BF

(8) 'we didn't see her/him'

a. hatu-e-m-on-a (> hetwemona)
NegSM1PL-NegPst-OM3SG-see-BF

b. hatu-e-m-on-a (> hetwemona)
NegSM1PL-NegPst-OM3SG-see-BF

c. hatu-ku-mw-on-a
NegSM1PL-NegPst-OM2SG-see-BF

(9) 'a child didn't buy a book'

a. mwana ha-e-nunu-ɭa kitabu (> henunuɭa kitabu)
child1 NegSM3SG-NegPst-buy-BF book7

b. mwana ha-e-nunu-ya buku (> henunuya buku)
child1 NegSM3SG-NegPst-buy-BF book5

c. mtoto ha-ku-nunu-a kitabu
child1 NegSM3SG-NegPst-buy-BF book7

Kama tunavyoona, katika Kitumbatu-Gomani na Kichaani kunatokea mabadiliko kadhaa ya sauti. Katika lahaja hizi mbili kiambishi-njeo cha ukanushi cha wakati uliopita ni '-e-', yaani vokali, kwa hivyo kwa mfano katika sentensi (8)a na (8)b vokali ya kwanza ya kiambishi-kiima 'hatu-' yaani 'a' imebadilika kuwa vokali 'e' kwa kupata taathira ya kiambishi-njeo '-e'. Tunaonyeshwa mabadiliko hayo ya sauti katika Jedwali la 1. Halafu kama tunavyoona katika mfano wa (5), kiambishi-tamati kinayo konsonanti [ɭ] katika Kitumbatu-Gomani na konsonanti [j] katika Kichaani kabla ya vokali vilevile ili kuepusha mfululizo wa vokali tatu wakati mzizi wa kitenzi unapoishia na vokali.

＜Jedwali la 1: Mabadiliko ya Sauti katika Kauli ya Ukanushi wa Wakati Uliopita＞

| Nafsi/Ngeli | Mabadiliko ya Sauti | | |
|---|---|---|---|
| 1SG | si-e- | > | se- |
| 2SG | hu-e- | > | hwe- |
| 3SG | ha-e- | > | he- |
| 1PL | hatu-e- | > | hetwe- |
| 2PL | ham-e- | > | hemwe- |
| 3PL | hawa-e- | > | hewe- |
| 3 | hau-e- | > | hewe- |
| 4 | hai-e- | > | heye- |
| 5 | hali-e- | > | helye- |
| 6 | haya-e- | > | heye- |
| 7 | haki-e- | > | heche- |
| 8 | havi-e- | > | hevye- |
| 9 | hai-e- | > | heye- |
| 10 | hazi-e- | > | heze- |
| 11 | hau-e- | > | hewe- |
| 14 | hau-e- | > | hewe- |
| 15 | haku-e- | > | hekwe- |
| 16 | hapa-e- | > | hepe- |
| 17 | haku-e- | > | hekwe- |
| 18 | hamu-e- | > | hemwe- |

## 2.2 Kitenzi chenye Silabi Moja

Sasa tuangalie muundo wa sentensi za njeo iliyopita zenye kitenzi chenye silabi moja.

(10) ‘a child fell down’

a. mwana ka-g-u
child1 SM3SG-fall-V

b. mwana ka-g-u
child1 SM3SG-fall-V

c. mtoto a-li-anguk-a
child1 SM3SG-Pst-fall-BF

(11) ‘children fell down’

a. wana wa-g-u
children2 SM3PL-fall-V

b. wana wa-g-u
children2 SM3PL-fall-V

c. watoto wa-li-anguk-a
children2 SM3PL-Pst-fall-BF

(12) ‘a bag fell down’

a. mkoba u-g-u
bag3 SM3-fall-V

b. mkoba u-g-u
bag3 SM3-fall-V

c. mkoba    u-li-anguk-a
bag3    SM3-Pst-fall-BF

(13) ‘bags fell down’

a. mikoba    i-g-u
bags4    SM4-fall-V

b. mikoba    i-g-u
bags4    SM4-fall-V

c. mikoba    i-li-anguk-a
bags4    SM4-Pst-fall-BF

(14) ‘a stone fell down’

a. bwe    li-g-u
stone5    SM5-fall-V

b. jibwe    li-g-u
stone5    SM5-fall-V

c. jiwe    li-li-anguk-a
stone5    SM5-Pst-fall-BF

(15) ‘stones fell down’

a. mabwe    ya-g-u
stones6    SM6-fall-V

b. mabwe    ya-g-u
stones6    SM6-fall-V

c. mawe    ya-li-anguk-a
stones6    SM6-Pst-fall-BF

(16) ‘a knife fell down’

a. kisu    ki-g-u
knife7    SM7-fall-V

b. kisu    ki-g-u
knife7    SM7-fall-V

c. kisu    ki-li-anguk-a
knife7    SM7-Pst-fall-BF

(17) ‘knives fell down’

a. visu    vi-g-u
knives8    SM8-fall-V

b. visu    vi-g-u
knives8    SM8-fall-V

c. visu    vi-li-anguk-a
knives8    SM8-Pst-fall-BF

(18) ‘a stick fell down’

a. fimbo    i-g-u
stick9    SM9-fall-V

b. fimbo    i-g-u
stick9    SM9-fall-V

c. fimbo i-li-anguk-a
stick9 SM9-Pst-fall-BF

(19) ‘sticks fell down’
a. fimbo zi-g-u
sticks10 SM10-fall-V
b. fimbo zi-g-u
sticks10 SM10-fall-V
c. fimbo zi-li-anguk-a
sticks10 SM10-Pst-fall-BF

(20) ‘a thread fell down’
a. ɭugwe u-g-u
thread11 SM11-fall-V
b. uzi u-g-u
thread11 SM11-fall-V
c. uzi u-li-anguk-a
thread11 SM11-Pst-fall-BF

(21) ‘threads fell down’
a. nyugwe zi-g-u
threads10 SM10-fall-V
b. nyuzi zi-g-u
threads10 SM10-fall-V
c. nyuzi zi-li-anguk-a
threads10 SM10-Pst-fall-BF

Kitenzi kinachotumika katika mifano (10)~(21) ni ‘kugwa’ kwa Kitumbatu-Gomani na Kichaani, ingawa kwa Kiswahili Sanifu ni ‘kuanguka’. Wakati kinapotumiwa kitenzi chenye silabi moja, inawezekana kusema kiambishi-tamati ‘V’ kinaathirika na kuendana na konsonanti ya mzizi wa kitenzi, lakini jambo hilo bado halijafafanuliwa, inahitajika utafiti wa dhati juu ya mabadiliko ya sauti.

Sasa tuangalie ikoje kauli ya ukanushi inayotumia kitenzi chenye silabi moja.

(22) ‘a child didn’t fall down’
a. mwana ha-e-gw-a (< hegwa)
child1 NegSM3SG-NegPst-fall-BF
b. mwana ha-e-ku-gw-a (< hekugwa)
child1 NegSM3SG-NegPst-Inf-fall-BF
c. mtoto ha-ku-anguk-a
child1 NegSM3SG-NegPst-fall-BF

(23) ‘children didn’t fall down’
a. wana hawa-e-gw-a (< hewegwa)
children2 NegSM3PL-NegPst-fall-BF

b. wana hawa-e-ku-gw-a (< hewekugwa)

children2 NegSM3PL-NegPst-Inf-fall-BF

c. watoto hawa-ku-anguk-a

children2 NegSM3PL-NegPst-fall-BF

(24) 'a bag didn't fall down'

a. mkoba hau-e-gw-a (< hewegwa)

bag3 NegSM3-NegPst-fall-BF

b. mkoba hau-e-ku-gw-a (< hewekugwa)

bag3 NegSM3-NegPst-Inf-fall-BF

c. mkoba hau-ku-anguk-a

bag3 NegSM3-NegPst-fall-BF

(25) 'bags didn't fall down'

a. mikoba hai-e-gw-a (< heyegwa)

bags4 NegSM4-NegPst-fall-BF

b. mikoba hai-e-ku-gw-a (< heyekugwa)

bags4 NegSM4-NegPst-Inf-fall-BF

c. mikoba hai-ku-anguk-a

bags4 NegSM4-NegPst-fall-BF

(26) 'a stone didn't fall down'

a. bwe hali-e-gw-a (< helyegwa)

stone5 NegSM5-NegPst-fall-BF

b. jibwe hali-e-ku-gw-a (< helyekugwa)

stone5 NegSM6-NegPst-Inf-fall-BF

c. jiwe hali-ku-anguk-a

stone5 NegSM5-NegPst-fall-BF

(27) 'stones didn't fall down'

a. mabwe haya-e-gw-a (< heyegwa)

stones6 NegSM6-NegPst-fall-BF

b. mabwe haya-e-ku-gw-a (< heyekugwa)

stones6 NegSM6-NegPst-Inf-fall-BF

c. mawe haya-ku-anguk-a

stones6 NegSM6-NegPst-fall-BF

(28) 'a knife didin't fall down'

a. kisu haki-e-gw-a (< hechegwa)

knife7 NegSM7-NegPst-fall-BF

b. kisu haki-e-ku-gw-a (< hechekugwa)

knife7 NegSM7-NegPst-Inf-fall-BF

c. kisu haki-ku-anguk-a

knife7 NgeSM7-NegPst-fall-BF

(29) 'knives didn't fall down'

a. visu havi-e-gw-a (< hevyegwa)

knives8 NegSM8-NegPst-fall BF

b. visu havi-e-ku-gw-a (< hevyekugwa)

knives8 NegSM8-NegPst-Inf-fall-BF

c. visu havi-ku-anguk-a

knives8 NegSM8-NegPst-fall-BF

(30) ‘a stick didn’t fall down’

a. fimbo hai-e-gw-a (< heyegwa)

stick9 NegSM9-NegPst-fall-BF

b. fimbo hai-e-ku-gw-a (< heyekugwa)

stick9 NegSM9-NegPst-fall-BF

c. fimbo hai-ku-anguk-a

stick9 NegSM9-NegPst-fall BF

(31) ‘sticks didn’t fall down’

a. fimbo hazi-e-gw-a (< hezegwa)

sticks10 NegSM10-NegPst-fall-BF

b. fimbo hazi-e-ku-gw-a (< hezekugwa)

sticks10 NegSM10-NegPst-Inf-fall-BF

c. fimbo hazi-ku-anguk-a

sticks10 NegSM10-NegPst-fall-BF

(32) ‘a thread didn’t fall down’

a. ɭugwe hau-e-gw-a (< hewegwa)

thread11 NegSM11-NegPst-fall-BF

b. uzi hau-e-ku-gw-a (< hewekugwa)

thread11 NegSM10-NegPst-Inf-fall-BF

c. uzi hau-ku-anguk-a

thread11 NegSM10-NegPst-fall-BF

(33) ‘threads didn’t fall down’

a. nyugwe hazi-e-gw-a (< hezegwa)

threads10 NegSM10-NegPst-fall-BF

b. nyuzi hazi-e-ku-gw-a (< hezekugwa)

threads10 NegSM10-NegPst-Inf-fall-BF

c. nyuzi hazi-ku-anguk-a

threads10 NegSM10-NegPst-fall-BF

Kama tuonyeshavyo katika mifano ya (22)~(33), Kitumbatu-Gomani hakihitaji kiambishi cha -ku- ya kitenzi kisoukomo ingawa Kichaani kinahitaji. Na kama tulivyoona kwa Jedwali la 1, kunatokea mabadiliko ya sauti katika kiambishi-kiima cha ukanushi kwa ajili ya taathira ya kiambishi cha ukanushi cha wakati uliopita katika Kitumbatu-Gomani na Kichaani. Katika kauli ya ukanushi kiambishi-tamati hakiendani na vokali ya mzizi wa kitenzi kinachotumiwa bali ni kiishio cha msingi tu katika Kitumbatu-Gomani na Kichaani.

Sasa tuangalie mfano mwingine wa kitenzi chenye silabi moja ulio na kiambishi-yambwa.

(34) 'I gave her/him a book'

a. ni-m-k-i kitabu
SM1SG-OM3SG-give-V book7

b. ni-m-p-i buku
SM1SG-OM3SG-give-V book5

c. ni-li-m-p-a kitabu
SM1SG-Pst-OM3SG-give-BF book7

Kutokana na mfano wa (34) tunafahamu kwamba msamiati wa kitenzi 'give' ni tofauti katika Kitumbatu-Gomani kwa kulinganisha na Kichaani na Kiswahili Sanifu, yaani 'kuka' na si 'kupa'. Na hata tukitumia kiambishi-yambwa hakutokei tofauti na kauli isiyo na kiambishi-yambwa, yaani hakitokei kiambishi-njeo cha wakati uliopita wala kiishio hakiwi cha msingi. Tuangalie kauli ya ukanushi katika mfano wa (35).

(35) 'I didn't give her/him a book'

a. si-e-m-k-a kitabu (< semka)
NegSM1SG-NegPst-OM3SG-give-BF book7

b. si-e-m-p-a buku (< sempa)
NegSM1SG-NegPst-OM3SG-give-BF book5

c. si-ku-m-p-a kitabu
NegSM1SG-NegPst-OM3SG-give-BF book7

## 2.3 Kauli ya Wakati Uliopita yenye Kitenzi 'be'

(36) 'twenty years ago I had a cow'

a. myaka ishirini i-yo-pit-a ni-vu na ng'ombe
years4 20 SM4-Rel4-pass-BF SM1SG-bePst with cow9

b. miyaka ishirini i-yo-pit-a ni-evu (> nyevu) na ng'ombe
years4 20 SM4-Rel4-pass-BF SM1SG-bePst with cow9

c. miaka ishirini i-li-yo-pit-a ni-li-ku-w-a na ng'ombe.
years4 20 SM4-Pst-Rel4-pass-BF SM1SG-Pst-Inf-be-BF with cow9

(37) 'three years ago you were a student'

a. myaka mi-tatu i-yo-pit-a ku-vu mwanafuzi
years4 AP4-three SM4-Rel4-pass-BF SM2SG-bePst student1

b. miyaka mi-tatu i-yo-pit-a ku-evu (> kwevu) mwanafuzi.
years4 AP4-three SM4-Rel4-pass-BF SM2SG-bePst student1

c. miaka mi-tatu i-li-yo-pit-a u-li-ku-w-a mwanafunzi.
years4 AP4-three SM4-Pst-Rel4-pass-BF SM2SG-Pst-Inf-be-BF student1

Kama tunavyoona katika mifano ya (36) na (37), katika kauli ya njeo ya wakati uliopita yenye kitenzi ‘be’ kuna tofauti kubwa sana baina ya Kitumbatu-Gomani, Kichaani na Kiswahili Sanifu. Katika Kitumbatu-Gomani kitenzi ‘be’ yaani ‘kuwa’ umbo lake limebadilika kabisa na kuwa -vu, na katika Kichaani umbo lake limebadilika kuwa -evu. Lakini bado haijafafanuliwa vizuri, kwa hivyo haieleweki maumbo hayo yamebadilika vipi kutoka -wa na kwenda -vu ama -evu.

## 3. Hitimisho

Katika makala hii tumeangalia miundo ya sentensi za Kitumbatu-Gomani za njeo iliyopita kwa kulinganisha na sentensi za Kichaani na Kiswahili Sanifu. Kama tulivyotaja juu, tofauti kubwa sana iliyoko baina ya Kitumbatu-Gomani na Kiswahili Sanifu inatokea katika sentensi za njeo iliyopita na tuseme kinyume cha hayo Kitumbatu-Gomani na Kichaani kinafanana katika sentensi hizo za njeo iliyopita, ingawa baadhi ya msamiati unatofautiana.

Na tena, kama tulivyoona hapo juu, umbo hili la njeo iliyopita linaonekana katika lahaja ya Kimtang’ata pia kwa mjibu wa makala ya Whiteley (1959), kwa hivyo unahitajika utafiti zaidi na zaidi juu ya lahaja nyingine za Kiswahili si katika kisiwa cha Unguja tu bali katika eneo la bara hasa mkabala na kisiwa cha Unguja ili kufafanua uhusiano kamili uliopo baina ya lahaja zenyewe.

Na isitoshe, inasemekana kuwa ili kubainisha kwamba kuna tofauti ama ulinganifu kama huu hasa baina ya Kitumbatu na lahaja zinazozungumzwa katika vijiji vingine vilivyotambulikana kwamba vilijengwa na wanaotoka kisiwa cha Tumbatu, tunahitaji kufanya utafiti zaidi na zaidi katika eneo kubwa la Mkoa wa Kaskazini, kisiwa cha Unguja, na kulinganisha na kuchambua matokeo yake.

* Utafiti wangu huu uliendeshwa kwa msaada wa kifedha wa Wizara ya Elimu ya Japani wa mwaka wa kielimu 2016-2018. Mradi wetu wa utafiti (Namba ya mradi:(C) T16K026700, Kiongozi wa mradi:TAKEMURA Keiko, Profesa, Chuo Kikuu cha Osaka) unaitwa ‘Utafiti wa Lahaja za Kiswahili, Kisiwani Unguja - Kufafanua Tofauti za Kisarufi na Kimsamiati’.

## Shukrani

Utafiti wa mara hii usingekamilika bila ya msaada wa mhojiwa Bi. ‘M’ ambaye ndiye wifi yangu wa tatu wa huko kijijini Chaani. Mbali na utafiti wangu, kila mara ninapofika Chaani ananisaidia na kunijali sana. Namtakia kila la kheri katika maisha yake. Na lazima nimtaje bibi yangu wa Chaani, kila mara nilisaidiwa na mhojiwa Marehemu Bi. ‘M’ - Mungu amlaze pahala pema peponi - aliyekuwa akikaa katika mtaa mmoja wa Chaani. Nisingekutana naye bila shaka

nisingeweza kuandika makala hii, ninamshukuru kwa dhati yangu hasa. Mwezi wa 8 mwaka 2016 niliweza kuzuru kaburini kwake, kumbukumbu nyingi zilinijia kichwani na nilijihakikishia kuwa sitamsahau maisha, amina!

Na tena kila mara nilisaidiwa sana na msaidizi wangu Mwl. ‘H’ pamoja na familia yake. Nilikaa na familia yake kwa muda wote nilipokuwa Chaani. Kwa msaada wao mkubwa niliweza kufanya utafiti wangu bila ya tatizo lolote, ninawashukuru mno. Halafu lazima nitaje jina lake Mwl. Zainabu kwa msaada wake mkubwa. Amenipitia na kunirekebishia makala hii kama kawaida. Ninamshukuru sana sana.

Mwishoni niongeze kutaja kwamba ikiwa kuna makosa ama kasoro ya maandiko ya makala hii, bila shaka ni wajibu wangu, na si wajibu wao mhojiwa na wasaidizi wangu.

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| - | mpaka wa mofimu |
| 1SG, 1PL | nafsi ya kwanza-umoja, nafsi ya kwanza-wingi |
| 2SG, 2PL | nafsi ya pili-umoja, nafsi ya pili-wingi |
| 3SG, 3PL | nafsi ya tatu-umoja, nafsi ya tatu-wingi |
| AP | kiambishi cha kivumishi |
| APPL | kiambishi-nyambulishi cha kutendea |
| BF | kiishio cha msingi |
| Inf | kiambishi cha -ku- ya kitenzi kisoukomo |
| Neg | kiambishi-ukanushi |
| OM | kiambishi-yambwa |
| Prs | wakati uliopo |
| Pst | wakati uliopita |
| Rel | kiambishi-kirejeshi |
| SM | kiambishi-kiima |
| V | kiambishi-tamati cha njeo ya wakati uliopita |

## Marejeo

Bryan, M. A. 1959. “Swahili Group”. *The Bantu Languages of Africa*. pp.126-129. Oxford University Press.

Mkude, Daniel J. 1983. “Mtawanyiko wa Lahaja za Kiswahili”. *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I - Lugha ya Kiswahili*. pp.62-83. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nurse, D. & T. J. Hinnebusch. 1993. *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. University of California Press.

Stigand, C. H. 1915. *A Grammar of Dialectic Changes in the Swahili Language*. Cambridge University Press.

Stude, Traute. 1995. “Language Change and Language Maintenance in the Island of Tumbatu”. *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. pp.83-117. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Takemura, Keiko. 2014. “On Subjunctive and Imperative Forms of Kichaani”. *Swahili & African Studies* No. 25. pp.120-129. (in Japanese)

――. 2015. “Miundo ya Dhamira Matilaba na Dhamira Amri katika Kichaani”. *Swahili & African Studies* No.26. pp.170-180.

――. 2016. “Miundo ya Sentensi zenye Kitenzi ‘-wa’ katika Kichaani - Kulinganisha na Kiswahili Sanifu”. *Swahili & African Studies* No.27. pp.53-63.

Whiteley, W. H. 1956. *Ki-mtang’ata: A Dialect of the Mrima Coast - Tanganyika*. East African Swahili Committee, Makerere College, Kampala.